

Haraka haraka haina Baraka: Mazoezi**Zoezi la Kwanza: Toa maana ya msamiati huu**

- i) Kushona
- ii) Kupima
- iii) Fundi nguo
- iv) Kubana
- v) Vitambaa
- vi) Kuharakisha

Zoezi la Pili: Tunga sentensi kwa kutumia maneno katika swali la Kwanza**Zoezi la Tatu: Chagua jibu lililosahihi;**

- i) Kuluthumu na Amina walienda wapi?
 - A: Walienda sokoni
 - B: Walienda harusini
 - C: Walienda kwa fundi nguo
- ii) Rafiki hawa wawili walitaka
 - A: Kushonewa nguo
 - B: Kupimwa nguo
 - C: Kuchukua nguo
- iii) Kwanini Amina alitaka nguo yake ishonwe haraka?
 - A: Alitaka apendeze zaidi ya rafikiye
 - B: Aliona atachelewa harusini
 - C: Alihitaji kuenda sokoni
- iv) Siku ya harusi ilipofika
 - A: Amina alipendeza sana
 - B: Kuluthumu alipendeza
 - C: Nguo ya Amina haikumtosha vizuri

- v) Hii si mojawapo ya methali inayoweza kuelezea kisa hiki
- A: Haraka haraka haina Baraka
- B: Subira huvuta heri
- C: Pole pole ndio mwendo

Zoezi la Nne: Kweli au Si kweli

- i) Amina na Kuluthumu walishonewa nguo na mpita njia
- ii) Amina alikuwa na haraka ya kwenda sokoni
- iii) Amina alitaka kuichukua nguo yake siku iliyofuata
- iv) Fundi hakushona nguo zote mbili vizuri
- v) Wanawake walitaka nguo zishonwe kwa ajili ya kwenda kilioni
- vi) Methali haraka haraka haina Baraka inakaribiana sana kimaana na Subira huvuta heri.

Zoezi la 5: Kuandika muhtasari

Andika Muhtasari wa igizo hili kama unamwadithia mtu mwingine.

Zoezi la 6: Kuelezea maana

Elezea maana ya methali hii “haraka haraka haina baraka” kama Ilivyotumika katika hadithi hii.

Zoezi la 7: Kulinganisha na kutofautisha

Linganisha na tofautisha maana ya methali hizi- subira huvuta heri na haraka haraka haina Baraka

Zoezi la 8: Jibu Swalii hili

Taja methali au msemo wa Kiingereza unayofanana na methali hii
Unaweza kuelezea methali hiyo hutumikaje?

Zoezi la 9: Jibu Swalii hili

Andika kisa kifupi kingine ambacho kinaweza kuelezea methali "haraka haraka haina Baraka"

Zoezi la 10: Jibu swalii hili

Jaribu kuigiza methali hii ili kufanya mazoezi ya kuongea na kukumbuka